# NENO LA MWISHO WAKATI WA PASAKA

Watu kadhaa wa msingi katika hadithi ya kusulubishwa na kufufuka kwa Yesu hawakukubaliana kuhusu lolote, lakini walikubaliana kuhusu hili: hadithi ya Yesu ilikuwa imekwisha.

Ponsyo Pilato aliamini kwamba yeye alikuwa mtu mwenye neno la mwisho kwenye mambo yote yaliyokuwa yakitendeka katika eneo lake. Lilikuwa eneo lenye misukosuko katika dunia ya Rumi lakini, licha ya mazingira ya changamoto, Pilato alizoea kuwa na mamlaka yasiyowekewa maswali. Kama akiamua mtu asiye na hatia anahitajika kuuwawa ili amani idumu, itakuwa hivyo. Alimtoa Yesu asulubiwe, na zoezi la kuua msalabani lilitendeka kwa amri yake. Baadaye, baada ya kusikia habari za kifo cha Yesu, Pilato alitoa agizo lake la mwisho kwa viongozi wa dini. 'Haya mnao walinzi, nendeni mkalinde kadiri mjuavyo' (Mathayo 27:65). Kimsingi palikuwa na vifungo vitatu kwenye kaburi la Yesu: jiwe kubwa liliviringishwa mbele, muhuri rasmi ulikuwa onyo kuu na walinzi wenye silaha walilinda kuhakikisha hayupo atakaye ingilia kati. Pilato alikuwa na uhakika kwamba ndiye mwenye mamlaka ya mwisho juu ya hadithi ya Yesu.

Mariamu, mama yake Yesu, alitambua uchungu wa kumuona mpendwa wake akiteseka. Aliangalia upinzani dhidi ya Yesu ulipokuwa unakua, na bila shaka alihofu siku baada ya siku kwamba kitu kibaya kitatokea. Hatimaye , maadui wa Yesu wenye nguvu walikwenda kunyume naye. Baada ya kukamatwa kwake, uvumi unaweza kuwa ulisambazwa kuhusu kupigwa, kuteswa na mateso aliyokabiliana nayo. Anaweza kuwa alijisikia hana uwezo, akavunjika mno kufahamu kwamba mwanae alikuwa anapitia maumivu ya namna hii. Mariamu angeweza kuyatoa maisha yake, kuyaokoa ya mwanae, lakini hilo halikuwa linawezekana. Alichoweza kufanya mama yake ni kusimama karibu naye hadi mwisho mchungu, akiwa hataki mwanae akabiliane na mwisho wa maumivu akiwa peke yake. Alikuwepo, karibu ya msalaba, Yesu alipokuwa anavuta pumzi ya mwisho (Yohana 19:25). Akiwa amejawa na kukata tamaa, Mariamu alikuwa na uhakika kifo chake cha kutisha kilikuwa ukurasa wa mwisho wa hadithi ya Yesu.

Petro alitambua kwamba huduma yake ilikuwa imekwisha na, kwa kweli, alielewa ilitakiwa kwisha. Hata hivyo, alikuwa amemkana Yesu, sio mara moja, sio mara mbili, ila mara tatu. Pale pale ambapo Yesu alikuwa anamhitaji zaidi, alikuwa kaanguka vibaya. Baada ya jogoo kuwika, na Petro kukumbuka maneno ya Yesu – kwamba kabla jogoo hajawika, Petro atakuwa amemkana Yesu mara tatu – aliinamisha kichwa chake kwa kushindwa akalia kwa uchungu (Mathayo 26:75). Petro alikuwa hajawahi kukata tamaa namna hii. Licha ya kuwaahidi marafiki zake na rabi kwamba hata kama wengine watamkana, yeye hata thubutu, ilimchukua msichana mfanya kazi kumfanya afunguke na kumong'onyoka. Katika kumkana Yesu, Petro alikuwa amepoteza huduma ambayo ilikuwa imekuwa ni maisha yake na furaha yake katika miaka mitatu iliyopita. Pamoja na kifo cha rafiki yake hadharani msalabani, pamoja na kumkana kwake mwenyewe mara tatu kwamba yeye sio mwanafunzi wake, Petro aliamini kwamba sehemu yake katika hadithi ya Yesu ilikuwa imekwisha.

Lakini hadithi ya Yesu ilikuwa bado haijaisha. Wote walisahau kitu muhimu sana: Ni Mungu ndiye mwenye neno la mwisho siku zote.

Katika siku ile ya kwanza ya asubuhi ya Pasaka, wakati kila mmoja aliamini hadithi yote ya Yesu imekwisha kuandikwa, baba wa mbinguni aliandika sura yenye nguvu kuliko zote mpaka sasa. Jiwe kubwa liliviringishwa litoke, mhuri ulivunjwa na walinzi walishikwa na hofu (Mathayo 28:2-4).Haya yote yalidhihirisha kwamba hakuna watu au nguvu hapa duniani zinaweza kumzuia Mungu asiwe na neno la mwisho. Yesu alifufuka, yu hai tena, na kwa sababu ya ukweli huo wenye nguvu, kila kitu

kilibadilika. Pilato na mazingira aliyoamuru haya kuwa na mamlaka ya mwisho juu ya Mwana wa Mungu au wafuasi wake. Mariamu aliweza kuona kifo cha mwanae sio kama mwisho, bali kama sehemu ya hadithi inayoendelea ya neema ya Mungu inayolazimisha kwa wanadamu. Na katika siku zilizofuata, Petro aligundua kwamba huduma yake ya kabla ya kumkana Yesu itakuwa hata kubwa zaidi ya jinsi alivyotegemea au kudhania (Yohana 21:15-19).

Huenda unakabiliana na wakati wa changamoto katika maisha yako wakati huu. Uwe na hakika wa hili: Mungu ndiye mwenye neno la mwisho, na hayupo adui au mazingira yanayoweza kusimama kinyume na neno la Mungu mwenye uwezo wote.

Huenda mtu unayempenda mno anaugua sana, nawe unajiona kuwa huna uwezo wa kutosha wa kumuondolea uchungu wake au kumponya maumivu yake. Kumbuka, Mungu ndiye mwenye neno la mwisho, neno hilo litakuwa limejaa na neema, na matumaini, na ushindi wa mwisho.

Huenda, kama Petro, haujisikii tena kuwa unathamani ya kutumiwa na Mungu. Huenda kuna wakati ulimwacha na una hakika yeye haja kuacha wewe. Uwe na hakika ya hili: Mungu atakuwa na neno la mwisho, nalo litakuwa neno lenye nguvu ya kurejesha nakufanya upya. Na nani anajua? Labda, kama Petro, utagundua kwamba huduma yako yenye mguso zaidi ingali inakuja.

Maombi yangu kwako, na kwa Jeshi la Wokovu zima, ni kwamba Pasaka hii itatangaza upya kwamba hadithi ya Yesu bado haijaisha, na kwamba Mungu siku zote ndiye mwenye neno la mwisho, lenye ushindi. Litakuwa neno la ushindi linalotukumbusha kwamba Mungu ni mkuu kuliko adui yeyote anayesimama dhidi yake. Litakuwa neno la nguvu lenye neema na matumaini kwa waliovunjika moyo na wanaoumia. Na litakuwa neno la urejesho, linalotukumbusha kwamba haipo dhambi iliyo kubwa zaidi ya neema yake inayokomboa.

Mungu atakuwa na neno la mwisho, nalo litakuwa neno la ushindi!

Pasaka ya Furaha, na Mungu akubariki.

Lyndon Buckingham
**Jenerali**